



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



**TANGAZO LA MWALIKO WA WATAZAMAJI WA UCHAGUZI WA NDANI  
KATIKA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA MBARALI NA  
MADIWANI KATIKA KATA SITA ZA TANZANIA BARA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Mbarali, Mkoa wa Mbeya na Madiwani katika kata sita za Tanzania Bara. Uchaguzi huo utafanyika siku ya Jumanne tarehe 19 Septemba, 2023 katika Jimbo tajwa na kata sita ambazo ni: -

Na.	Kata	Halmashauri
1.	Nala	Jiji la Dodoma
2.	Mfaranyaki	Manispaa ya Songea
3.	Mtyangimbole	Wilaya ya Madaba
4.	Mwaniko	Wilaya ya Misungwi
5.	Old Moshi Magharibi	Wilaya ya Moshi
6.	Marangu Kitowo	Wilaya ya Rombo

Kwa mujibu wa kanuni ya 18 (3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 16(3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za (Uchaguzi wa Madiwani) mwaka 2020, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa mwaliko kwa watazamaji wa uchaguzi wenye nia ya kutazama uchaguzi.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inakaribisha maombi kutoka kwa taasisi na asasi nchini zenyе nia ya kutazama uchaguzi mdogo wa Ubunge Jimbo la Mbarali na kata sita zilizopo katika halmashauri sita za Tanzania Bara kama ilivyoainishwa kwenye jedwali.


Taasisi na asasi zenyne nia ya kutazama uchaguzi huo ziwasilishe maombi kwa kutumia anuani (*link*) ifuatayo <https://oms.nec.go.tz>

Barua ya maombi pamoja na mambo mengine itatakiwa kuainisha mambo yafuatayo: -

- i. Anuani kamili ya taasisi au asasi husika;
- ii. Mahali ambapo taasisi au asasi husika inafanya kazi (Physical address);
- iii. Shughuli ambazo zinafanywa na taasisi au asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili;
- iv. Maeneo ambayo taasisi au asasi inapenda kwenda kutazama uchaguzi;
- v. Idadi ya watu ambao taasisi au asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na majina na taarifa zao binafsi;
- vi. Majina na namba za simu za viongozi wa taasisi au asasi husika kama yalivyoandikwa katika hati za usajili;
- vii. Ikiwa taasisi au asasi inahusisha watendaji wa kimataifa, viongozi wawili ambao taarifa zao zitawasilishwa ni lazima wawe watanzania;
- viii. Kuambatisha nakala au kivuli cha hati ya usajili wa taasisi au asasi husika; na
- ix. Kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika.

**Maombi yatapokelewa kuanzia tarehe 5 hadi 12 Agosti, 2023.**

Imetolewa leo tarehe 05.....Agosti, 2023 na:

  
Kailima, R.K  
MKURUGENZI WA UCHAGUZI